Matokeo ya utafiti wa mradi wa Minara ya Maji, Londiani, Msitu wa Mau

Lengo:

Kutambua iwapo na ni kwa njia gani vyama vya msitu wa jamii na jumuiya za watumiaji rasilimali zinashirikiana katika kusimamia rasilimali za msitu na maji

Douglas Bwire, Esther Mwangi, Sylvia Rotich

Maelezo ya jumla ya msitu wa Londiani

Msitu wa Londiani unapatikana katika sehemu ya magharibi ya msitu wa Mau, na una eneo la hekta 9015.50. Chama cha msitu wa jamii (CFA) cha Londiani kina wanachama wapatao 2500 na makundi ya watumiaji wafuatao: wachungaji wa mifugo, wakusanyaji wa kuni, wapunguzaji matawi ya miti, wafugaji nyuki, wasimamizi wa maji, vitalu vya miti, wakataji nyasi, kilimo cha samaki, utamaduni, na wakusanyaji madawa. Jumuiya ya watumiaji wa rasilimali ya maji (WRUA) ya Kipchorian hupatikana katika sehemu ya bonde ndogo ya Kipchorian, eneo la kilomita za mraba 162.5, na ina wanachama 200. Wanaume watatu kutoka Kondamet na Koyumgaa walikuwa wanachama wa CFA na pia wa WRUA.

Mchakato wa utafiti

Vyama viwili vya kijamii (CBO) chini ya CFA (Borop na Tulwap) vilichaguliwa. Tulichagua makundi ya watumiaji yafuatayo: ufugaji, usimamizi wa maji, vitalu vya miti, ufugaji wa nyuki na ukusanyaji kuni. Tulifanya mijadala ya vikundi maalum (focus group discussions) 38 na wanachama na wasio wanachama wa CFA, na mahojiano muhimu na wenye ufahamu wa kutosha kuhusu mambo katika jamii (key informant interviews) 6 na viongozi wa vikundi vya watumiaji na WRUA. Tulijadiliana na wanaume na wanawake 371 kwa jumla ambao walitenganishwa kwa umri kama inavyoonyeshwa kwenye Kielelezo 1.



Kielelezo 1. Asilimia ya washiriki wanaume na wanawake katika mijadala ya vikundi maalum.



Kielelezo 2. Idadi ya mijadala ya vikundi maalum kwa kila kikundi cha watumiaji Londiani.

Mtazamo wa jamii wa hali na mabadiliko ya msitu na maji

Maoni yalikuwa tofauti kati ya wanaume na wanawake kuhusu hali za msitu katika kipindi cha miaka 5 hadi 10 iliyopita. Mtazamo wa wanaume vijana na wazee ni kwamba Kupungua kwa ukubwa wa msitu wa asili unatokana na uchomaji moto wa msitu, ukataji miti na kukosa kupanda mingine, na kuipa nafasi mradi wa Uanzishwaji wa Upangaji na Mpango wa Uboreshaji wa Maisha (PELIS). Wanawake walihisi kuwa mazingira ya msitu yaliimarika kwa sababu PELIS iliwawezesha kutunza miti iliyopandwa nao wakilimia mazao yao sambamba. Wanawake walitaja kuwa utekelezaji wa sheria kali ili kulinda msitu ulichangia kuboreshwa kwa hali. Wanaume vijana walitaja kuwa uchomaji mkaa (kutokana na ukosefu wa ajira) ulichangia uharibifu wa msitu.

Kwa kipindi cha miaka 5 hadi 10 iliyopita viwango vya maji vimepungua na baadhi ya vijito imekauka na mchangatope kuongezeka kwenye mito. Mabadiliko ya viwango vya maji yametokana na uharibifu wa msitu, uchomaji moto ndani ya msitu ulioacha udongo bila uoto, upandaji wa mkaratusi katika kinga za mito, ongezeko la mahitaji ya maji, na matumizi ya mbolea kwenye mashamba ya kilimo na karibu na mito. Kinyume na haya, wanachama wengine wa CFA wanahisi kuwa ubora wa maji umeboreka, na kuwa mwavuli wa msitu umeongezeka. Wanachama wa WRUA waliona upunguaji wa viwango vya maji na ongezeko la mchangatope unaotokana na kilimo kwenye kinga za mito.

Kiungo kati ya misitu na maji: Wanajamii wanao uelewa wa uhusiano kati ya rasilimali za msitu na za maji. Washiriki wa mjadala katika vikundi maalum walitaja upunguaji wa viwango vya maji unaohusiana na mabadiliko ya mwavuli wa msitu. Pia, wale ambao walitaja uboreshaji wa rangi ya maji na viwango vyake walihusisha mabadiliko hayo na shughuli za kurejesha msitu.

Uongozi

Uongozi wa CFA una wanaume wawili (mwenyekiti na katibu) na mwanamke mmoja (mweka hazina). Kuna usawa wa jinsia katika uongozi katika ngazi ya vikundi vya watumiaji. Katika vikundi 10 vya watumiaji waliohusika katika mijadala ya vikundi maalum, wanawake 10 na wanaume 8 walikuwa katika nafasi za uongozi.

Wanaume huchaguliwa kwa sababu wanaaminika kuwa mameneja bora zaidi, wanaohusika na wenye ujasiri wakati wa kufanya maamuzi. Wanawake huchaguliwa kwa sababu wao ni waaminifu, wawazifu na fedha ni wasikilizaji wema, wenye ujuzi wa mfumo wa PELIS, na husambaza taarifa kwa urahisi. Wanawake washiriki hawakuona tofauti yoyote kati ya uongozi wa wanaume na wanawake. Kwa mujibu wao, wanaume na wanawake wote wanao uwezo wa kuchukua nafasi za uongozi.

Uchaguzi wa CFA unafanyika, kimsingi, kila baada ya miaka mitano. Hata hivyo, uchaguzi umefanyika mmoja tu tangu CFA kuundwa. Baadhi ya wanachama wa CFA walisema hawakujua idadi ya uchaguzi



zilizofanyika. Kipindi kwa ofisi katika WRUA ni miaka mitano na uchaguzi wa mwisho ulifanyika mwaka 2017. WRUA ina ngazi mbili za uongozi: menejimenti na kamati ndogo tano za ununuzi, fedha, ufuatiliaji na tathmini, ukame na usimamizi wa mafuriko, na shughuli za kimaisha. Katika ngazi ya menejimenti kuna wanaume 3 na wanawake 2, na katika kamati ndogo kuna wanaume 13 na wanawake 12.

Shughuli kwa pamoja kati ya CFA na WRUA

Londiani CFA na Kipchorian WRUA hazijawahi tekeleza shughuli kwa pamoja. Wanachama wa CFA hawazifahamu shughuli za WRUA. Wanachama wote wa CFA na wale wa WRUA walionelea kuwa eneo lao pamoja na uanachama vinazuia uwezekano wa shughuli kwa pamoja. Wanachama wa CFA walisema kuwa wanachama wa WRUA wanapaswa kuishi kwenye maeneo yaliyo kando ya mito na vijito. Wanachama wa WRUA nao wakasema kuwa wanachama wa CFA wanapaswa kukaa katika nyanda za juu karibu na msitu. Ingawa hii ndiyo ilivyokuwa hali, wanachama wa CFA na wa WRUA walikubaliana kuwa kuna haja ya vyama hivyo viwili kuendesha kazi zao kwa pamoja.

Sehemu zilizopendekezwa za kushirikiana

Wajumbe wote wa Londiani CFA na Kipchorian WRUA walikubaliana kufanya kazi kwa pamoja katika shughuli zifuatazo:

- Kuregesha ilivyokuwa hali ya eneo la chanzo cha maji kwa kupanda miti ya asili (kama vile *lamaiywet, ndereret na emtit*) katika maeneo ya misitu na mashamba
- Kuzuia kilimo kandokando ya mito, na kushirikisha jamii katika kukata miti ya mkaratusi kando ya mito na vijito.
- Kuelimisha jamii kuhusa uwekezaji mbadala katika vyanzo vya maji katika kaya, k.m. uvunaji wa maji ya mvua na uchimbaji wa visima.

Wakati wa mradi wa utafiti, WRUA na CFA walikuwa wamesha anzisha mpango wa kazi wa kupanda miti 10,000 katika maeneo mawili ya Mt. Blanket na Cheboror. Mpango huu ulitimizwa baada ya mafunzo ya kujenga uwezo katika mbinu ambazo zinaendeleza uhifadhi shirikishi wa rasilimali za misitu na maji.

Kushiriki katika CFA na WRUA

Wengi wa wanachama wa CFA wanahisi kuwa hawashiriki katika kikundi cha watumiaji kwa sababu kwa kawaida huwa hawaalikwi. Wanachama hawa walipendekeza kuwa mawasiliano ya wazi yanahitajika kutoka kwa viongozi. Viongozi wa CFA kwa kawaida hushauriana na viongozi wa vikundi vya watumiaji kuhusu masuala ya hatari ya moto msituni, upandaji miti na PELIS. Wanachama wanaalikwa kuhudhuria mikutano ya kila mwezi ya WRA ili kupata taarifa kuhusu shughuli zinazotekelezwa. Mwaliko unatolewa pamoja na ajenda, tarehe na taarifa kuhusu pahala pa mkutano. Baada ya mikutano yao, viongozi wa CFA wa vikundi vya watumiaji huwaeleza wanachama yaliyojadiliwa. Mikutano kwa pamoja kati ya WRUA na CFA haijawahi kufanyika.

Hitimisho

Wanachama wa vikundi vya CFA na WRUA huko Londiani wana uelewa kwamba shughuli zinazoathiri mwavuli wa misitu zinaathiri pia ubora na viwango vya maji. Mitazamo hii ilitofautiana kwa hali ya mabadiliko. Wanaume wakiona upunguaji wa mwavuli wa msitu, na wanawake wa vikundi vya watumiaji vya CFA wakionelea kuwa mfumo wa PELIS uliboresha hali za msitu.

Wanachama wa WRUA walieleza kuwa kupungua kwa viwango vya maji na uchafuzi wa maji vilitokana na mmomonyoko wa udongo kupitia ukulima kando ya mito, kung'oka kwa mimea karibu na mito, upandaji wa miti ya mkaratusi kwenye maeneo kando ya mito na vijito na matumizi ya mbolea katika mashamba. Wanachama wa WRUA walikuwa na ufahamu wa mikutano na walihisi kuwa wanashiriki zaidi kwa mikutano hii kuliko kwa mikutano ya CFA ambapo kulikuwa na pengo la mawasiliano kati ya viongozi na wanachama.

Uratibu haupo kati ya CFA na WRUA. Moja ya sababu ni kwamba eneo lilionekena kuwa na upana mkubwa kiasi cha kuzuia ushirikiano. Hata hivyo, wanachama wa vikundi hivi wanakubaliana kuwa ni muhimu kutekeleza shughuli zingine kwa pamoja na wakatoa mapendekezo vile watashirikiana.

Mapendekezo

- Kuongeza uwezo wa wanachama wa CFA na wa WRUA ili kupanua wigo wa shughuli zao. Hatua hii itawezesha Kipchorian WRUA kuzingatia shughuli za usimamizi wa maji na uhifadhi wa maeneo kando ya mito na vijito, na vilevile uelewa wa umuhimu wa kuhifadhi msitu kama eneo la bonde.
- Kuongeza uelewa wa ushirikiano katika bonde ili 'mipaka' ya kijiografia ya hivi vyama viwili isiwe kizuizi. Masuala haya hatimaye yatasaidia kuvileta pamoja hivi vyama viwili na kuviratibu katika shughuli za uhifadhi wa misitu na maji.
- Kuimarisha uwezo wa viongozi katika ujuzi, kwa mfano wa mawasiliano, ili kuboresha utendaji wa vyama.
- Kuandaa mikutano ya mipango kwa pamoja kati ya Londiani CFA na Kipchorian WRUA ili kuboresha uratibu.

Na ufadhili wa

Federal Ministry for Economic Cooperation and Development

Lancaster University

KENYA Forest Service

Water Resources Authority

the green belt movement

Kenya Water Towers Agency